on accessibility and supply of She said palliative care ... important that all providers prioritize quality first.

DAILY NEWS Page 4.

# Ex-fisheries officer seeks JPM's help in lost job

A FORMER Assistant Fisheries Officer with the Ministry of Fisheries in Bunda District, Mara region is appealing to President John Magufuli to intervene in a case where he was allegedly fired 24 years ago unreasonably.

Emmanuel Mayira (74) claims that he was first suspended and subsequently fired in 1996 by the then area District Director under the order of the then District Commissioner.

He alleged that as an office tasked to arrest suspected illegal fishermen and their equipment, he arrested some only for them to be freed without any charge and their fishing tools returned.

"We were five (read officers), but I wonder why my juniors in the case were reinstated and late paid their benefits," he said.

According to Mayira, when he was 50 years he received a termination letter while attending two separate security meetings, unknowingly organized by the district commissioner.

He said that during the meeting, the DC lambasted and accused him for blackmailing fishermen in his name.

A document seen by the 'Daily News' indicated the DC displaying at least 11 fishermen having signed a petition that Mr Mayira had some bribe from them.

"We demanded during the District Security meeting that such fishermen claiming to have been asked to part with money in the name of the DC's directive come forward, but none turned out, making the security committee rule that the allegation was baseless and we deserved to return to our duty," he added.

However, he said his work was exemplary and earned two awards as the best employee of the year, but it was unfortunate that he was framed for a crime he never committed.

"Iattemptedtoseekjustice in high offices including at the Regional Commissioner and Commission for Civil Servants, where I was once awarded on merits, but never got my work back as well as benefits.

"But I believe, the President would intervene and let justice takes its course, because he is a man of the people dishonoured in the society. I have made more than ten attempts to reach him, but all in vain," said the former officer.

Commenting on the case, Elisante Mbilo, Director of Service in the Office of the President Public Service Management and Good Governance speaking to the Daily News yesterday, said such matters could still be resolved but with proper documents at hand.

"I suggest that you send the person with all his documents to our office in Dodoma so that our team of legal experts can advise where necessary," he said.

Scanned with CamScanner

MTANZANIA UK 10.

PICHA: MPIGAPICHA WETU



**UFUGAJI KISASA: Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), Angellah Kairuki (wa pili kushoto) akitazama ng'ombe wa maziwa katika shamba la la ASAS lililoko nje kidogo ya mji wa Iringa. Kushoto ni Mkurugenzi wa Kampuni ya hiyo, Feisal Abri.**

MBEYA

UHALIFU

SUMBAWANGA

# Anayedaiwa kuiba mtoto wa dada yake mbaroni

**Na GURIAN ADOLF**

**JESHI** la Polisi mkoani Rukwa, linamshikilia mwanamke mmoja (jina limehifadhiwa) mkazi wa Kijiji cha Msata mkoani Pwani kwa tuhuma za kuiba mtoto mwenye umri wa wiki moja, kisha kuchoma godoro alilokuwa amelalia ili kupoteza ushahidi.

Tukio hilo lilitokea Juni 11, mwaka huu saa 2;30 za usiku eneo la Namanyere wilayani Nkasi.

Mtuhumiwa anadaiwa kuiba mtoto huyo kwa kwa ndugu yake, Samia Ruhusa(35) mkazi wa Namanyere.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Rukwa, Justine Masejo alisema siku ya tukio hilo mtuhumiwa alimpigia simu mama wa mtoto na kumwambia yupo Dar es Salaam, amemtumia fedha za matumizi kupitia mtandao wa simu ,aende akazitoe usiku ili zimsaidie kipindi hiki ambacho amejifungua.

Baada ya mama wa mtoto kuambiwa hivyo, aliondoka nyumbani kwake

Scanned with CamScanner

**MSAADA: Mkurugenzi wa Rasilimali Watu na Utalawa wa Benki ya TPB, Diana Myonga (katikati) akikabidhi msaada wa mabati 100 kwa aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalumu kwa Mkoa wa Singida, Aysharose Matembe (wa nne kulia) mwishoni mwa wiki iliyopita kukamilisha ujenzi wa shule za sekondari na msingi mkoani humo.**

# Wafanyabiashara mifugo Handeni walia na changamoto za mnada

**Na TUNU NASSOR**
**-HANDENI**

WAFANYABIASHARA wa mifugo katika mnada wa Handeni wameimba serikali kuzitatua changamoto zilizopo katika mnada huo ili kuwarahisishia utendaji kazi wao.

Akizungumza na MTANZANIA hivi karibuni, Mwenyekiti wa wafanyabiashara hao, Abdi Mhandeni changamoto hizo zinachangia kushindwa kufikia malengo yao ya kibiashara.

Alisema katika mnada huo wamekuwa wakitozwa Sh 6,500 kwa ng'ombe mmoja lakini fedha hizo hazisaidii uboreshwaji wa miundombinu ya mnada huo.

"Changamoto tulizonazo tunahitaji suluhu kwakuwa hata wafanyabiashara wa ng'ombe wana miaka zaidi ya miwili mlango wa kuingilia kwenye boma umevunjika lakini hakuna jitihada zozote zinazofanyika wakati ushuru unakusanywa," alisema Mhandeni.

Alisema hadi sasa mipaka ya mnada huo hainekani vizuri jambo ambalo linasababisha kila kukicha mgogoro.

Naye mfanyabiashara Waziri Gumbo, alisema Serikali ifikirie kukarabati miundombinu ya machinjio ili kutoa fursa ya kupata wateja wengi zaidi tofauti na hivi sasa.

Alisema miundombinu mibovu jambo ambalo linasababisha magari kuingia kwa tabu mnadani.

"Tunachangamoto nyingi hapa lakini kubwa ni kuharibika kwa zizi la kupakizia ambalo limekuwa likisababisha mifugo inayohifadhiwa kutoroka mara kwa mara," alisema Gumbo.

Kwa upande wake Nasib Kalabaka, alisema mnada huo hauna uzio uko wazi kila upande na kusababisha kushindwa kuwakamata wahalifu.

Alisema hata mifugo wakitoroka inawawia vigumu kumkamata katika mnada ambao hauna uzio.

"Wakati wa upakiaji mifugo kwenye magari lango la kupitia limeharibika hivyo ni rahisi kwa ng'ombe kutoroka na kumsababishia hasara mnunuzi ambaye tayari amelipia ushuru," alisema Kalabaka.

Scanned with CamScanner

sambamba na kuongeza programu na kozi mbalimbali ili kukidhi matak-

MTANZANIA UK 18

SOKO

# Bei ya samaki soko la Feri yazidi kupaa

CHRISTINA GAULUHANGA
-DAR ES SALAAM

**BEI ya samaki katika soko la kimataifa la Feri imezidi kupaa kutokana na kuwapo kwa upepo unaosababisha samaki kukimbia.**

Akizungumza na MTANZANIA Mwenyekiti wa soko hilo, Mbaraka Kilima alisema samaki wamefikia Sh 60,000 kwa ndoo ndogo.

Alisema hali hiyo imesababisha wafanyabiasahara wa samaki kupata changamoto ya bei ya kuuza mitaani.

"Hali hii itakuwa ni ya muda mfupi baadaye itarejea kawaida kulingana na hali ya hewa itakavyokuwa," alisema Kilima.

Alisema zipo baadhi ya changamoto zinazolikabili soko hilo ambapo wanasubiri uzinduzi wa bodi ya soko kuzinduliwa ili waweke mikakati endelevu ya kuziondoa.

"Tumekuwa tukigawa vitambulisho vya utambuzi kwa wafanyabiashara lakini zoezi hili limesimama kusubiri uzinduzi wa bodi mpya," alisema Kilindi.

Alisema kutokana na uwapo wa ugonjwa wa Covid-19 soko hilo limeendelea kuchukua tahadhari zote za kujikinga kulingana na maelekezo ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na watoto.

"Tunashukuru Mungu kwa soko kuendelea kuchukua tahadhari za ugonjwa wa Covid-19 lakini bado kuna watu wanaokaidi kwa amadai kuwa ugonjwa huu umekwisha," alisema Kilima.



Scanned with CamScanner